# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI


1. Jina fupi na kuanza kutumika.

2. Marekebisho ya Sheria mbalimbali.


### SEHEMU YA PILI
### MAREKEBISHO YA SHERIA YA UMILIKI WA ARDHI, NAM. 12 YA 1992


3. Kusomwa.

4. Marekebisho ya kifungu cha 3.

5. Marekebisho ya kifungu cha 46.

6. Marekebisho ya kifungu cha 47.

7. Marekebisho ya kifungu cha 56.


### SEHEMU YA TATU
### MAREKEBISHO YA SHERIA YA MITAJI YA UMMA, NAM. 4 YA 2002


8. Kusomwa.

9. Marekebisho ya kifungu cha 6.

10 Marekebisho ya kifungu cha 8.

11. Marekebisho ya kifungu cha 27.

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTUMISHI WA UMMA, NAM. 2 YA 2011

12. Kusomwa.

13. Marekebisho ya kifungu cha 15.

14. Marekebisho ya kifungu cha 29.

15. Marekebisho ya kifungu cha 55.

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KUANZISHA AFISI YA TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR, NAM. 1 YA 2017

16. Kusomwa.

17. Marekebisho ya kifungu cha 32.

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA SHIRIKA LA NYUMBA LA ZANZIBAR, NAM. 6 YA 2014

18. Kusomwa.

19. Marekebisho ya kifungu cha 7.

20. Marekebisho ya kifungu cha 26.

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA, NAM. 4 YA 2015

21. Kusomwa.

22. Marekebisho ya kifungu cha 41.

## SEHEMU YA NANE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KUANZISHA OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI, NAM. 11 YA 2003.


23. Kusomwa.

24. Marekebisho ya kifungu cha 8.

25. Kuongezwa kifungu kipya cha 9A.


## JADWELI
## MWENENDO WA BODI
**(Chini ya kifungu cha 9A)**

## SEHEMU YA TISA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAKAMPUNI, NAM. 15 YA 2013


26. Kusomwa.

27. Marekebisho ya kifungu cha 2.

28. Marekebisho ya kifungu cha 3.

29. Marekebisho ya kifungu cha 19.

30. Marekebisho ya kifungu cha 129.

31. Marekebisho ya kifungu cha 155.

32. Marekebisho ya kifungu cha 191.

33. Marekebisho ya kifungu cha 195.

34. Marekebisho ya kifungu cha 216.

35. Marekebisho ya kifungu cha 235.

36. Marekebisho ya kifungu cha 241.

37. Marekebisho ya kifungu cha 248.

38. Kuongezwa kifungu kipya cha 279.

## SEHEMU YA KUMI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UNUNUZI NA UONDOWAJI WA MALI ZA UMMA, NAM. 11 YA 2016

39. Kusomwa.

40. Marekebisho ya kifungu cha 27.

41. Kuongezwa kifungu kipya cha 65A.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAFAO YA VIONGOZI MAALUM, NAM. 5 YA 2003

42. Kusomwa.

43. Marekebisho ya kifungu cha 6.

**SHERIA NAMBA 1 YA 2018**

**NIMESAINI**

**{DR. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

2 Januari, 2018

# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya mwaka 2017 na itaanza kutumika mara baada ya kukubaliwa na Rais.

Marekebisho ya Sheria mbalimbali.

**2.** Sheria zilizotajwa katika sehemu mbalimbali za Sheria hii zinarekebishwa kwa namna zinavyoelezwa katika sehemu husika.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UMILIKI WA ARDHI, NAM. 12 YA 1992

Kusomwa.

**3.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Umiliki wa Ardhi, Nam. 12 ya 1992, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria mama".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**4.** Kifungu cha 3 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo cha (6) kama ifuatavyo:

"(6) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (2) na (3) cha kifungu hiki, Rais akiridhika na ushahidi uliopelekwa mbele yake, atafuta uamuzi uliotolewa na Waziri unaohusiana na ugawaji wa Ardhi na uamuzi wa Rais utakuwa wa mwisho na hautohojiwa na Mahkama yoyote.

Marekebisho ya kifungu cha 46.

**5.** Kifungu cha 46 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo cha (5) kama ifuatavyo:

"(5) Mkataba wa ukodishwaji wa ardhi ya umma uliyotolewa chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, utafutwa mara baada ya kufutwa au kusitishwa kibali cha uwekezaji".

Marekebisho ya kifungu cha 47.

**6.** Kifungu cha 47(1) cha Sheria mama kinafutwa na kuweka vifungu vidogo vipya vya (1) na (2) vifuatavyo:

"(1) Mkataba wa ukodishaji wa ardhi ya Umma uliotolewa chini ya masharti ya Sehemu hii hautazidi miaka tisini na tisa ambayo itatolewa kwa utaratibu wa awamu kwa miaka isiyozidi thelathini na tatu kwa kila kipindi."

"(2) Waziri kwa kushauriana na Waziri anaehusika na uwekezaji atatathmini maendeleo ya uwekezaji kabla ya kuongeza muda wa mkataba wa ukodishaji wa ardhi".

Marekebisho ya kifungu cha 56.

7. Kifungu cha 56 ya Sheria mama kinafutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

"Haki ya kusitisha kwa maslahi ya umma.

Waziri anaweza kusitisha haki ya matumizi ya Ardhi kwa msingi wa maslahi ya umma kwa kulipa fidia kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 63 cha Sheria hii".

**SEHEMU YA TATU**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MITAJI YA UMMA, NAM. 4 YA 2002**

Kusomwa.

**8.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mitaji ya Umma, Nam. 4 ya 2002, katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria mama".

Marekebisho ya kifungu cha 6.

**9.** Kifungu cha 6(4) cha Sheria mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu cha 6A kama ifuatavyo:

"Muda wa wajumbe wa Bodi

6A. Mwenyekiti wa Bodi atakaa madarakani kwa muda wa miaka minne na wajumbe wengine kwa muda wa miaka mitatu kutoka tarehe waliyoteuliwa na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine".

Marekebisho ya kifungu cha 8.

**10.** Kifungu cha 8 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa:

(a) kubadilisha nambari ya kifungu cha 8 kuwa 8(1); na

(b) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (2) kama ifuatavyo:

"(2) Kila agizo la Bodi litakalofanywa kuhusu kuwekeza, kukopa fedha, mishahara na maposho litakalotolewa kwa Shirika litawasilishwa Baraza la Mapinduzi na Waziri anayehusika kwa ajili ya kuidhinishwa, kabla ya agizo hilo halijatekelezwa na Shirika".

Marekebisho ya kifungu cha 27.

**11.** Kifungu cha 27 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

"27. Waziri anayehusika mara tu baada ya kupokea taarifa ya mwaka, kwanza ataiwasilisha taarifa hiyo Baraza la Mapinduzi kabla hajawasilisha Baraza la Wawakilishi yenye mambo yafuatayo:

(a) taarifa ya mpango mkakati wa Shirika kwa mwaka huo na miaka miwili inayofuata;

(b) taarifa ya mwaka na taarifa ya ukaguzi wa hesabu za Shirika kwa mwaka uliopita; na

(c) taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu juu ya taarifa za fedha.

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTUMISHI WA UMMA, NAM. 2 YA 2011

Kusomwa.

**12.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya 2011, ambapo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria mama".

Marekebisho ya kifungu cha15.

**13.** Kifungu cha 15(1) cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (1) na kuweka kifungu kidogo kipya kifuatacho:

"15(1) Kila Wizara itawasilisha taarifa ya utekelezaji kwa Katibu Mkuu Kiongozi ambaye naye atawasilisha kwa Rais, si zaidi ya miezi minne baada ya kumalizika mwaka wa fedha.

Marekebisho ya kifungu cha 29.

**14.** Kifungu cha 29 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (3) na kuweka kipya kama ifuatavyo:

"(3) Ripoti iliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki:

(a) itapitia utekelezaji wa utumishi wa umma wa mwaka unaofanyiwa mapitio;

(b) itabainisha hatua zilizochukuliwa au zinazotakiwa kuchukuliwa kutatua matatizo yanayohusiana na utekelezaji huo;

(c) itaeleza maendeleo ya hatua zilizobainishwa katika ripoti ya mwaka uliopita;

(d) itajumuisha mapendekezo ambayo Kamisheni itaona yanafaa kwa kuimarisha Utumishi wa Umma na Maafisa wa Utumishi wa Umma; na

(e) itajumuisha taarifa nyengine yoyote kama Rais atakavyohitaji.

Marekebisho ya kifungu cha 55.

**15.** Kifungu cha 55 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongeza vifungu vidogo vipya vya (8) na (9) mara baada ya kifungu kidogo cha (7) kama ifuatavyo:

"(8) Agizo lolote la Bodi kuhusiana na uwekezaji, kukopa fedha, mishahara na maposho lililotolewa na Bodi ya Wakurugenzi au Bodi ya Ushauri ya Wakala litawasilishwa Baraza la Mapinduzi na Waziri husika kwa ajili ya kuidhinishwa, kabla ya agizo hilo kutekelezwa na Wakala.

(9) Mwenyekiti wa Bodi atakaa madarakani kwa muda wa miaka minne na wajumbe wengine kwa muda wa miaka mitatu kutoka tarehe walioteuliwa na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine".

(b) kurekebisha nambari za vifungu vidogo vya (8) hadi (12) kwa mpangilio wake.

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KUANZISHA AFISI YA TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR, NAM. 1 YA 2017

Kusomwa.

**16.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi, Nam. 1 ya 2017, ambapo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria mama".

Marekebisho ya kifungu cha 32.

**17.** Kifungu cha 32(1) cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno "Sheria ya Utumishi wa Umma" na badala yake kuweka neno "Rais".

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA SHIRIKA LA NYUMBA LA ZANZIBAR, NAM. 6 YA 2014

Kusomwa.

**18.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Shirika la Nyumba, Nam 6 ya 2014, ambapo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria mama".

Marekebisho ya kifungu cha 7.

**19.** Kifungu cha 7 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo cha (5) mara baada ya kifungu kidogo cha (4) kama ifuatavyo:

> "(5) Bila ya kujali masharti yoyote ya Sheria hii, Shirika halitofanya mauzo ya jengo lolote bila ya ridhaa ya Baraza la Mapinduzi".

Marekebisho ya kifungu cha 26.

**20.** Kifungu cha 26 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kuongeza vifungu vidogo vipya vya (5) na (6) mara baada ya kifungu kidogo cha (4) kama ifuatavyo:

> "(5) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki, makubaliano yoyote ya kukodisha nyumba baina ya Shirika na mtu yeyote hayatozidi muda wa miaka mitano, na makubaliano hayo yanaweza kuingiwa upya baada ya kukamilika kipindi cha awali.
>
> (6) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki, Shirika linaweza kuingia mkataba wa muda mrefu na mtu yeyote wa kukodisha jengo kwa zaidi ya miaka mitano baada ya kupata idhini ya Baraza la Mapinduzi".

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA, NAM. 4 YA 2015

Kusomwa.

**21.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Nam. 4 ya 2015, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria mama".

Marekebisho ya kifungu cha 41.

**22.**-(1) Kifungu cha 41 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno "baada ya kuidhinishwa na Baraza la Wawakilishi" na badala yake kuweka maneno "na kuwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi kwa taarifa".

(2) Baraza litakuwa na uwezo wa kutoa maelekezo juu ya taarifa iliyowasilishwa na Waziri kutokana na marekebisho yaliyofanyika kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

## SEHEMU YA NANE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KUANZISHA OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI, NAM. 11 YA 2003

Kusomwa.

**23.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Nam. 11 ya 2003, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria mama".

Marekebisho ya kifungu cha 8.

**24.** Kifungu cha 8(1)(e) cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kuongeza maneno yafuatayo mwishoni mwa kifungu hicho:

"kwa kuzingatia jinsia".

Kuongezwa kifungu kipya cha 9A.

**25.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 9A mara baada ya kifungu cha 9 kama ifuatavyo:

"Mwenendo wa Bodi. 9A. Mwenendo na mambo mengine yanayohusu Bodi utakuwa kama itakavyoelezwa katika Jadweli la Sheria hii".

## JADWELI
## MWENENDO WA BODI
## (Chini ya kifungu cha 9A)

Muda wa wajumbe wa Bodi.

**1.**-(1) Mwenyekiti wa Bodi atakaa madarakani kwa muda wa kipindi cha miaka minne na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine.

(2) Mbali ya wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, Wajumbe wengine wa Bodi watashika madaraka kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine.

Vikao vya Bodi.

**2.**-(1) Bodi itakutana katika vikao vya kawaida mara moja kila baada ya miezi mitatu na inaweza kukutana wakati wowote itakapotokea haja ya kukutana kwa ajili ya kutekeleza kazi zake.

(2) Vikao vyote vya Bodi vitaitishwa na Mwenyekiti au ikiwa hayupo vitaitishwa na Makamu Mwenyekiti.

(3) Mwenyekiti au ikiwa hayupo Makamu Mwenyekiti ataitisha kikao cha dharura cha Bodi baada ya kupokea maombi ya maandishi yaliyowekwa saini na zaidi ya nusu ya wajumbe wa Bodi, na kikao hicho kitaitishwa ndani ya siku ishirini na moja baada ya kupokea maombi hayo.

(4) Endapo wote wawili Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe waliohudhuria watateua mjumbe mmoja miongoni mwao kuendesha kikao na mjumbe atakayeteuliwa atakuwa na uwezo wa kutekeleza uwezo wa Mwenyekiti.

Akidi ya kikao.

**3.** Zaidi ya nusu ya idadi ya Wajumbe itakuwa ndio akidi ya kikao cha Bodi.

Uamuzi wa Bodi.

**4.**-(1) Bodi itafanya uamuzi kwa makubaliano na ikiwa makubaliano hayatafikiwa, uamuzi utafanywa kwa kupiga kura na endapo itatokea kura kuwa sawa, Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, uamuzi wa Bodi unaweza kufanywa kwa kuwasilisha agizo kwa maandishi kwa wajumbe wote ambapo kila mjumbe ataeleza mawazo yake kwa maandishi ikizingatiwa kwamba mjumbe yeyote anaweza kuomba uamuzi huo uakhirishwe na kujadiliwa kwenye kikao cha wajumbe wa Bodi.

(3) Azimio lililotiwa saini na Wajumbe waliopo Zanzibar kwa wakati huo, ambao sio chini ya wajumbe watano, litachukuliwa kama uamuzi wa Bodi uliofanywa kwenye kikao ikizingatiwa kwamba, mjumbe bila ya kujali kama aliweka saini katika azimio hilo anaweza kuomba jambo hilo liwasilishwe kwenye kikao cha Bodi kinachofuata.

Kumualika mtu kwenye kikao.

**5.** Bodi inaweza kumualika mtu ambaye sio mjumbe kuhudhuria majadiliano ya Bodi kama mtaalam lakini mtu huyo hatokuwa na haki ya kupiga kura.

Kumbukumbu za vikao vya Bodi.

**6.** Kumbukumbu za mwenendo wa vikao vya Bodi zitaidhinishwa kwenye kikao kinachofuata cha Bodi kwa kutiwa saini na Mwenyekiti na Katibu wa Bodi.

Utaratibu wa vikao.

**7.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kupanga mwenendo na taratibu za vikao na utekelezaji bora wa kazi zake pamoja na kamati za Bodi.

Kutaja mgongano wa maslahi.

**8.** Mjumbe yeyote ambaye atakuwa na maslahi ya moja kwa moja au vyenginevyo, katika ajenda au jambo linalojadiliwa na Bodi atalazimika kutaja maslahi hayo mbele ya Bodi na hatotakiwa kushiriki katika kujadili ajenda au jambo hilo.

Katibu wa Bodi.

**9.** Bodi itateuwa Mwanasheria mwenye sifa ambaye ni muajiriwa wa Afisi kuwa Katibu wa Bodi.

Kazi za Katibu

**10.** Katibu atawajibika kwa Bodi na atakuwa anawajibu wa kuhakikisha kwamba:

(a) kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi zinachukuliwa;

(b) taarifa sahihi na zinazojitosheleza za Bodi zinahifadhiwa;

(c) taarifa za vikao vya Bodi zinatolewa kwa Wajumbe;

(d) anatoa ushauri sahihi kwa Bodi pale unapohitajika; na

(e) anafanya kazi nyengine yoyote kama atakavyoagizwa na Bodi.

Kamati za Bodi.

**11.**-(1) Bodi inaweza katika utekelezaji wa kazi zake, kuanzisha Kamati yoyote kufanya kazi maalum kama itakavyoagizwa na Bodi.

(2) Mwenendo, vigezo na masharti ya utendaji kazi wa kamati utakuwa kama Bodi itakavyoelekeza.

Kujiuzulu na kusita kwa nafasi ya mjumbe.

**12.**-(1) Mwenyekiti au mjumbe mwengine yeyote wa Bodi, anaweza kujiuzulu kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa mamlaka ya uteuzi na kuanzia tarehe ya taarifa hiyo au ikiwa hakuna tarehe iliyoainishwa katika taarifa, kuanzia tarehe iliyopokelewa taarifa hiyo na mamlaka ya uteuzi, mjumbe huyo atasita kuwa mjumbe wa Bodi.

(2) Endapo mtu amesita kuwa Mwenyekiti au mjumbe wa Bodi, kwa sababu yoyote kabla ya kumalizika muda wake wa kushika madaraka ya ujumbe, mamlaka ya uteuzi itateua mtu mwengine kushika nafasi hiyo na mtu huyo atashika nafasi hiyo kwa kipindi kilichobaki katika kipindi kilichoachwa na mtangulizi wake.

(3) Endapo mjumbe atashindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya sababu ya msingi, Mwenyekiti wa Bodi atawasilisha taarifa hiyo kwa Waziri na Waziri atafuta uteuzi wa Mjumbe huyo na kuteua mjumbe mwengine kushika nafasi ya mjumbe huyo kwa kipindi kilichoachwa na mtangulizi wake.

Nafasi ya mjumbe kuwa wazi.

**13.**-(1) Nafasi ya mjumbe wa Bodi itakuwa wazi kwa:

(a) kushindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi, bila ya sababu ya msingi;

(b) kujizulu au kwa namna yoyote kupoteza sifa za kuwa mjumbe wa Bodi;

(c) kushindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu za kiafya ya mwili au akili; au

(d) kufariki;

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Jadweli hili yanayohusu akidi, Bodi inaweza kuendelea na kazi zake bila ya kujali nafasi ya mjumbe yeyote kuwa wazi na jambo au mwenendo wa Bodi hautobatilishwa kwa sababu za kutokea makosa ya uteuzi wa mtu ambaye amefanywa kuwa mjumbe.

Posho za Wajumbe.

**14.** Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi watalipwa posho kwa kiwango atakachoamua Waziri muda hadi muda baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya mambo ya Fedha.

## SEHEMU YA TISA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAKAMPUNI, NAM. 15 YA 2013

Kusomwa.

**26.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Makampuni Nam. 15 ya 2013, ambayo katika sehemu hii itajulikana kama Sheria Mama.

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**27.** Kifungu cha 2(1) cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongezwa ufafanuzi wa maneno mapya yafuatayo kwa mpangilio wa alfabeti:

"Shirika la pekee" maana yake ni Idara ya Umma iliyoundwa kwa Sheria au kwa amri ya Rais iliyochapishwa katika Gazeti Rasmi, kuwa endelevu na muhuri rasmi na uwezo wa kumiliki, kushikilia, kusimamia, na kuondoa uwekezaji, kushtaki na kushtakiwa kusimamia mikataba na nyaraka, kwa kutumia muhuri wake, kuingia mikataba inayoibana au inayoifunga na waendelezaji wake katika utekelezaji wa haki zake katika uwekezaji, ikijumuisha na uwezo wa kuwa na mali zisizohamishika na nyingine;

"Kampuni ya Serikali "maana yake ni kampuni yoyote ambayo angalau asilimia hamsini na moja ya hisa zilizolipwa zinamilikiwa na Serikali, ikijumuisha kampuni tanzu ya Serikali;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na maswala yanayohusu usajili wa makampuni

"Shirika la Kisheria" maana yake ni shirika lolote ambalo linajumuisha shirika la umma na shirika pekee lililoundwa kwa Sheria lakini haijumuishi

kampuni iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Makampuni, ambapo hisa zote za Kampuni zinamilikiwa na shirika la kisheria au mashirika ya kisheria mawili au zaidi;

(b) kufutwa na kuwekwa ufafanuzi wa neno "Mrajis" kama ifuatavyo:

"Mrajis" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji aliyeteuliwa chini ya Sheria ya Wakala wa Usajili Biashara na Mali Zanzibar;

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**28.**-(1) Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufutwa kifungu kidogo cha (2) na kuwekwa badala yake kifungu kidogo kipya kama ifuatavyo:

(2) Mtu yeyote anaweza kuunda kampuni ya dhima yenye ukomo itakayojulikana kama kampuni binafsi ya mtu mmoja kwa kuweka jina lake katika katiba ya kampuni na kwa kutekeleza masharti ya Sheria ya Makampuni.

(b) kuongezwa vifungu vidogo vipya vya (4), (5) na (6) kama ifuatavyo:

(4) Shirika la Kisheria au Shirika Pekee linaweza kumiliki hisa zote za kampuni yoyote binafsi na kuwa mjumbe pekee wa kampuni hiyo.

(5) Endapo kampuni au Wakala chini ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki anamiliki hisa hupunguzwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria yoyote zinazohusiana na ubinafsishaji, masharti ya Sheria hii, au Sheria nyengine yoyote, kanuni za makampuni au mikataba au nyaraka nyengine za kampuni ambayo hisa zake zinaendelea kugawanyika, ambazo zinazohusiana na haki za awali za wanahisa, hazitatumika kuhusiana na kampuni hiyo.

(6) Waziri anaweza, kwa kuchapisha kwenye Gazeti Rasmi, kutoa msamaha kwa Shirika la Kisheria, Shirika Pekee au Kampuni ya Serikali kwa masharti yoyote ya Sheria hii.

Marekebisho ya kifungu cha 19.

**29.** Kifungu cha 19 cha Sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) katika kifungu kidogo cha (1) kunaingizwa maneno "kwa dhamana" baina ya neno "kampuni" na neno "ni"; na

(b) katika kifungu kidogo cha (2)(a) kunaingizwa maneno “kwa dhamana” baina ya neno "kampuni" na neno "ni"

Marekebisho ya kifungu cha 129.

**30.** Kifungu cha 129 (1) (c) cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa maneno "aya hiyo ya 5" na kuwekwa badala yake "kanuni".

Marekebisho ya kifungu cha 155.

**31.** Kifungu cha 155(3) cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa maneno "Sehemu ya III ya jadweli la saba" na kuwekwa badala yake neno "kanuni".

Marekebisho ya kifungu cha 191.

**32.** Kifungu cha 191 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya kama ifuatavyo:

"Kampuni ya mjumbe mmoja.

191. Mjumbe wa kampuni ya mjumbe mmoja hatokuwa, kwa hali yoyote, katibu wa kampuni hiyo".

Marekebisho ya kifungu cha 195.

**33.** Kifungu cha 195 (5) cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa maneno "moja kwa moja" na kuwekwa badala yake neno "Mkurugenzi".

Marekebisho ya kifungu cha 216.

**34.** Kifungu cha 216 (6) (a) cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kulirekebisha neno "fift" baina ya maneno "zaidi ya" na neno "siku" na kuweka badala yake maneno "kumi na tano".

Marekebisho ya kifungu cha 235.

**35.** Kifungu cha 235 (2) (a) na (d) cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa aya (a) na (d) na kuwekwa badala yake aya mpya ya (a) na (d) kama ifuatavyo:

(a) "mara moja amjuilishe Mrajis na kuitisha mkutano wa wadai kabla ya siku ya ishirini na nane kupita kuanzia siku aliyotoa maoni.

(d) katika kipindi kabla ya siku ambayo mkutano wa wadai haujafanyika atawapatia wadai taarifa zinazohusiana na hali ya kampuni kadri watakavyohitaji bila ya malipo.

Marekebisho ya kifungu cha 241

**36.** Kifungu cha 241 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya kama ifuatavyo:

Marejesho ya marekebisho yatakayowasilishwa kwa Mrajis na kampuni ya kigeni.

241.-(1) Endapo mabadiliko yamefanywa ndani ya:

(a) mkataba, Sheria, au katiba na kanuni za kampuni ya kigeni au hati rasmi ya kisheria kama ilivyoelezwa hapo awali; au

(b) wakurugenzi au katibu wa kampuni ya kigeni au maelezo yaliyomo kwenye orodha ya wakurugenzi na katibu; au

(c) majina au anuani za watu walioidhinishwa kupokea huduma kwa niaba ya Kampuni ya kigeni;

(d) anuani ya ofisi iliyosajiliwa au afisi kuu ya kampuni ya kigeni, au sehemu yake ya biashara iliyo ndani ya Zanzibar; au

(e) aina ya biashara ambayo kampuni ya kigeni itafanya biashara ndani ya Zanzibar, au jina litakalotumika katika biashara hiyo,

Kampuni hiyo, ndani ya siku sitini itawasilisha kwa Mrajis marejesho ya usajili ambayo yamejumuisha maelezo ya marekebisho.

(2) Endapo kampuni ambayo inahusiana na sehemu hii:

(a) itafungwa kwa amri ya Mahakama; au

(b) itafungwa kwa hiari kwa mujibu wa utaratibu chini ya Sheria hii ulioanza katika Mahakama ya nchi ambayo kampuni imeanzishwa,

kampuni hiyo ndani ya siku thelathini ya tarehe iliyotolewa amri hiyo au kuanza kwa mashauri ya kesi hiyo, kama hali itakavyokuwa, itawasilisha kwa Mrajis marejesho ambayo yana maelezo yanayohusiana na amri hiyo iliyotolewa au kuanza kwa mashauri hayo na kuyatangaza kwenye Gazeti Rasmi kama itakavyoelezwa na Waziri katika Kanuni.

Marekebisho ya kifungu cha 248.

**37.** Kifungu cha 248 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa maneno "aya ya 2" baina ya maneno "kifungu kidogo" na maneno "itakuwa na athari" katika masharti ya kifungu kidogo cha (1).

Kuongezwa kifungu kipya cha 279.

**38.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 279 baada ya kifungu cha 278 kama ifuatavyo:

"kubakiza

279. Bila kuathiri Sheria iliyofutwa chini ya kifungu cha 278 cha Sheria hii, kitu chochote kilichofanywa kwa mujibu wa masharti ya Sheria iliyofutwa kitachukuliwa kuwa kimefanywa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii".

### SEHEMU YA KUMI
### MAREKEBISHO YA SHERIA YA UNUNUZI NA UONDOWAJI WA MALI ZA UMMA, NAM. 11 YA 2016

Kusomwa.

**39.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ununuzi na Uondowaji wa Mali za Umma, Nam. 11 ya 2016, ambapo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria mama".

Marekebisho ya kifungu cha 27.

**40.** Kifungu cha 27(1) cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kuingiza neno "Wizara" baina ya maneno "kila" na "Idara" .

Kuongeza kifungu kipya cha 65A.

**41.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 65A mara baada ya kifungu cha 65 kama ifuatavyo:

"Katazo la kuuza jengo la Serikali.

65A. Mtu hatouza au hatoweka dhamira ya kuuza jengo lolote la Serikali bila ya kupata ridhaa ya Baraza la Mapinduzi".

### SEHEMU YA KUMI NA MOJA
### MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAFAO YA VIONGOZI MAALUM, NAM. 5 YA 2003

Kusomwa.

**42.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mafao ya Viongozi Maalum, Nam. 5 ya 2003, ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria mama".

Marekebisho ya kifungu cha 6.

**43.** Kifungu cha 6 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (3) mara baada ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki kama ifuatavyo:

6(3) Rais kwa kushauriana na Kamisheni ya Utumishi wa Umma na kwa Tangazo litakalochapishwa kwenye Gazeti Rasmi ataongeza Cheo na Afisi ya kiongozi atakayestahiki kupokea mafao ya uzeeni na kuweka kiwango au kima cha mafao ya uzeeni na stahiki nyengine.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 6 Disemba, 2017.

..................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi***

***Zanzibar.***